#WeweNdoFuture #TimizaWajibu

# HESLB Yako

Jarida la Mtandaoni la Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu | Toleo No. 14

Aprili - Juni 2024



# HESLB yaja na #Fichua kuwasaka wadaiwa sugu

**Ijumaa, Juni 28, 2024**

Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) leo (Ijumaa, Juni 28, 2024) imezindua Kampeni Maalumu inayolenga kuwashirikisha wananchi kwa kutumia simu na mitandao ya kijamii, kuwafichua wadaiwa sugu wa mikopo ya elimu ya juu.

Kampeni hiyo, inayofahamika kama #Fichua imezinduliwa jijini Dar es salaam na Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB Dkt. Bill Kiwia ambaye amesema kampeni hiyo itaendeshwa kwa miezi miwli kuanzia, Juni 28.

“Kampeni hii inalenga kuwashirikisha wananchi kutimiza jukumu la kizalendo la kuwafichua wadaiwa wa HESLB wenye kipato lakini hawajitokezi na kuanza kurejesha,” amesema Dkt. Kiwia katika mkutano na wanahabari.

“Tumeipa jina la #Fichua – KUWA HERO WA MADOGO ili kuhamasisha wananchi kushiriki katika urejeshaji wa mikopo iliyoiva ili iwanufaishe wengine – hatua ambayo bila shaka itawawezesha vijana wengi zaidi kupata elimu ya juu na wewe mwananchi kuwa SHUJAA wao,” ameongeza Dkt. Kiwia.

“Ili kutoa taarifa za wadaiwa, mwananchi anapaswa kutuma majina ya mnufaika, chuo alichosoma, eneo analofanya kazi, jina la kampuni anayofanyia kazi au anayomiliki na eneo ilipo kampuni hiyo,” amesema Dkt. Kiwia.

Ameongeza kuwa mwananchi anashauriwa kutuma taarifa hizo kwa barua pepe (fichua@heslb.go.tz); kutuma ujumbe wa WhatsApp (0739 66 55 33); kupiga simu kwenda 0736 66 55 33 kati ya saa 2:00 asubuhi hadi saa 10:00 jioni.

Njia nyingine ni pamoja na kutembelea tovuti www.heslb.go.tz na kuwasilisha taarifa kupitia kiunganishi cha ‘e-Mrejesho’. Pamoja na njia hizi, wananchi pia wanaweza kutuma ujumbe (DM – Direct Messages) kwenda Instagram, X au Facebook kwa jina la ‘HESLB Tanzania’ ZILIZOTHIBITISHWA na zenye ‘blue tick’.

Akizungumzia kampeni hiyo, Japhet Makyao, mwanafunzi wa mwaka wa tatu wa Shahada ya Udaktari na Upasuaji katika Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Kampala – Tanzania (KIUT) ameipongeza HESLB kwa ubunifu huo na kuwataka wadaiwa sugu wenye vipato kurejesha.

“Ukweli ni kuwa, mimi hadi sasa hivi mwaka wa tatu, bila Bodi ya Mikopo, nisingeweza kufika hapa … ningependa kuona waliowezeshwa kusoma na wana kipato, wajitokeze ili vijana wengine kama mimi wanufaike,” amesema Japhet mara baada ya uzinduzi huo.

Kwa upande wake, Khadija Sultan, mwanafunzi wa mwaka pili, Shahada ya Usimamizi wa Biashara katika Chuo Kikuu cha Tumaini – Dar es salaam (DarTU) ameishukuru Serikali kwa kumuwezesha kusoma na kuwaomba wadaiwa kumaliza kurejesha mikopo yao.

“Mimi ni yatima, nimepoteza wazazi wangu wote wawili nikiwa bado mdogo sana, bila Serikali nisingeweza kusoma kabisa … hivyo ninawaomba wale ambao hawajaanza kurejesha, au wanaorejesha kwa wasiwasi kuanza kurejesha,” amesema Khadija.

## NDANI...



04 JUMA: Asante Serikali kwa Samia Scholarship’



06 Dirisha Maombi ya mikopo 2024/2025 lafunguliwa

## JAMBO LETU



**Jacqueline Msuya**
*Mhariri*

# Msimu mpya wa maombi ya mikopo 2024/2025 umeanza

- **Unaomba mkopo? Zingatia mwongozo**

Tunaelekea kuingia mwaka mpya wa 2024/2025 na tayari tumewakaribisha waombaji wa mikopo ya elimu ambao wanatarajiwa kujiunga na vyuo vya kati na vya elimu ya juu katika mwaka mpya wa masomo utakaoanza mwishoni mwa mwezi Oktoba, 2024.

Dirisha la maombi ya mikopo kwa wanafunzi limefunguliwa kwa siku 90 kuanzia Juni 01, 2024 na litafungwa Agosti 31, 2024 kuwawezesha wanafunzi wanaotarajiwa kujiunga na vyuo vya elimu ngazi ya kati (stashahada) na vya elimu ya juu (shahada) kwa mwaka wa masomo 2024/2025. Maombi haya yanawahusisha wanafunzi waliohitimu kidato cha nne, cheti, kidato cha sita na stashahada ndani ya miaka mitano (2020 – 2024).

Kufunguliwa kwa dirisha la uombaji mikopo kwa mwaka wa masomo 2024/2025; kulitanguliwa na kutangazwa kwa mwongozo wenye taarifa za vigezo, masharti na utaratibu wa kuomba mikopo uliozinduliwa Mei 27, 2024 na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Profesa Adolf Mkenda ili kuwawezesha walengwa kuomba kwa usahihi na hatimaye kupangiwa viwango vya mikopo kulingana na stahili au hali yao ya kijamii na kiuchumi.

Ni muhimu kwa waombaji mikopo kuzingatia maelekezo yaliyomo katika Mwongozo wa Utoaji Mikopo na Ruzuku kwa mwaka wa masomo 2024/2025 kwa kila kundi (Stashahada, Shahada ya Awali, Stashahada ya juu ya Sheria kwa vitendo na Shahada za Umahiri na Uzamivu) ikitaja sifa, vigezo, ustahiki wa mwombaji, upangaji wa viwango vya mkopo kulingana na uhitaji na programu atakayodahiliwa.

Mwongozo wa utoaji mikopo ni taarifa ya wazi inayopatikana pia kupitia tovuti ya HESLB www.heslb.go.tz na kurasa zake za mitandao ya kijamii ili kuwawezesha waombaji, wazazi au walezi wao na wadau wengine muhimu kuusoma.

Baadhi ya nyaraka muhimu anazopaswa kuwa nazo mwombaji wa mkopo wa elimu ni cheti cha kuzaliwa, picha (passport size) ya mwombaji na ya mdhamini wake (mzazi au mlezi), kitambulisho cha mdhamini kimojawapo kati ya; Kitambulisho cha Taifa, Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi, Kadi ya Mpiga Kura, Leseni ya Udereva au Pasi ya kusafiria iliyotolewa na Serikali ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar .

Iwapo mwombaji atazingatia maelekezo, ni wazi ujazaji wa fomu ya maombi ambao ni kwa njia ya mtandao kupitia https://olas.heslb.go.tz unakuwa rahisi na anatumia muda mfupi kukamilisha vipengele vyote vinavyohitaji taarifa zake binafsi, za kitaaluma na za wazazi wake.

Uzoefu wa miaka ya nyuma umeonesha kuwa baadhi ya waombaji wanashindwa kujaza fomu za maombi kwa usahihi na ukamilifu kutokana na kutozingatia maelekezo yaliyomo katika Mwongozo husika. Mwaka 2022/2023 kwa mfano, kati ya maombi 100,260, maombi 2,997 hayakukamilika ikiwa ni sawa na asilimia 2.9%, wakati 2023/2024, kati ya maombi 126,361, maombi 6,093 hayakukamilika ikiwa ni sawa na asilimia 4.8%, HESLB Yako inatarajia kuwa maombi ya mwaka 2024/2025 yatakuwa na idadi kubwa ya wanafunzi waliojaza fomu zao kwa usahihi na kwa ukamilifu ndani ya muda wa siku 90 utakaotamatika Agosti 31, 2024.

**BODI YA UHARIRI**

**Mwenyekiti**
Dkt. Bill Kiwia

**Katibu**
Omega Ngole

**Mhariri**
Jacqueline Msuya

**Wajumbe**
Veneranda F. Malima
Eline Maronga
Jonathan Nkwabi
Ramadhan Namaru

**Designer**
+255 736 190 083



**Mawasiliano**
Jengo la PSSSF,
Barabara ya Makole,
eneo la Uhindini
S.L.P 984, Dodoma

**Simu:**
+255 758 067577
+255 739 067577

**Barua pepe:**
info@heslb.go.tz

**Tovuti:**
www.heslb.go.tz


HESLB
BODI YA MIKOPO
INVESTING IN THE FUTURE



# Wanafunzi 250,000 kunufaika 2024/2025

Nakukaribisha katika toleo la 14 la Jarida hili la Mtandao ili kupata kwa muhtasari yaliyojiri HESLB ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa majukumu ya kila siku na pia matukio muhimu ya kitaifa yaliyofanyika katika robo ya nne na ya mwisho ya mwaka 2023/2024.

Mwaka 2023/2024 ulikuwa wa mafanikio kwa HESLB na Serikali kwa ujumla katika kuhakikisha utoaji na urejeshaji wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu unafanyika kwa ufanisi.

Miongoni mwa mambo ya kukumbukwa kwa mwaka 2023/2024 ilikuwa kuanza kutolewa kwa mikopo kwa wanafunzi wa ngazi ya Stashahada (Diploma) na kuongezwa kwa kiwango cha fedha za kujikimu kwa siku kwa wanafunzi wa shahada za awali kutoka TZS 8,500 hadi TZS 10,000. Ni matarajio ya HESLB kuwa mwaka 2024/2025 utakuwa wa tija zaidi katika nyanja za utendaji, uwajibikaji na utoaji huduma kwa wateja ikiwa ni mwendelezo wa ufanisi wa mwaka 2023/2024.

Kipekee nitoe shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa utashi wake wa kuidhinisha ongezeko la bajeti kwa ajili ya kugharimia masomo ya wanafunzi wa elimu ya juu, hii inamaanisha kwamba wanafunzi wa Tanzania wana uhakika wa kusoma katika ngazi zote za elimu kwa ufadhili wa Serikali. Shukrani pia kwa usimamizi wa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda na Bodi ya Wakurugenzi wa HESLB ikiongozwa na Profesa Hamisi Dihenga; chini ya uongozi wao HESLB imekuwa imara zaidi.

Utoaji wa mikopo ya elimu ya juu nchini kwa sasa unawezeshwa na vyanzo vikuu viwili; Serikali Kuu na HESLB kwenye makusanyo ya mikopo kutoka kwa wanufaika. Mwaka 2023/2024, Serikali ilitenga TZS 786 bilioni, TZS 617 bilioni (78%) zilitolewa na Serikali Kuu na TZS 169 bilioni (22%) zilitoka HESLB kwenye makusanyo ya mikopo na kuwezesha kugharimia wanafunzi 224,056.

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (WyEST), yaliyowasilishwa na Profesa Adolf Mkenda Mei 07, 2024, Bungeni Dodoma yalielezea utekelezaji wa mpango wa mwaka 2023/2024, vipaumbele, mpango wa mwaka 2024/2025 na kuomba kuidhinishwa kwa jumla ya TZS 1.97 Trilioni, kati ya kiasi hicho, fedha za mikopo na ruzuku kwa wanafunzi wa elimu ya juu ni TZS 787 bilioni.

HESLB ikiwa miongoni mwa taasisi zilizo chini ya WyEST, imepewa kipaumbele kwa kuzingatia majukumu yake ya kuwawezesha wanafunzi wahitaji wa Kitanzania kugharimiwa masomo yao ya elimu ya juu katika fani mbambali. Fedha zilizotengwa bila shaka zitaongeza fursa za mikopo na ruzuku kwa wanafunzi wa vyuo vya kati na vya elimu ya juu kutoka wanufaika 224,056 (2023/2024) hadi kufikia wanufaika 250,000 (2024/2025).

Menejimenti ya HESLB imejipanga kuendelea kusimamia utoaji wa mikopo na ruzuku kwa wanafunzi wa vyuo vya kati na wa taasisi za elimu ya juu kulingana na ustahiki wa wanafunzi wahitaji wanaolengwa kunufaika kwa kugharimiwa masomo yao.

> *“kuanza kutolewa kwa mikopo kwa wanafunzi wa ngazi ya Stashahada (Diploma) na kuongezwa kwa kiwango cha fedha za kujikimu kwa siku kwa wanafunzi wa shahada za awali kutoka TZS 8,500 hadi TZS 10,000.*




# HESLB YASHEREHEKEA 'MIKOPO OPEN DAY' 2024

- **YATUNUKU WAAJIRI ZANZIBAR**

**Zanzibar, Juni 20, 2024**

Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB Dkt. Bill Kiwia ametoa tuzo za mwaka 2023/2024 kwa Taasisi kumi zilizopo Zanzibar kwa kutambua mchango wao katika urejeshaji wa mikopo ya wanafunzi na kufuata Sheria ya HESLB ipasavyo.

Akiongea katika hafla fupi ya utoaji tuzo ambayo pia ilitumika kusherehekea 'Mikopo Open Day' inayoadhimishwa kila mwaka kukumbuka kuanzishwa kwa taasisi hiyo mwezi Juni, 2004, Dkt. Kiwia alizipongeza taasisi zilizotunukiwa kwa kuonesha ushirikiano na umakini katika kutambua dhima ya HESLB ya kuhakikisha fedha zilizopeshwa kwa wanafunzi zinarejeshwa ili kuwezesha wanafunzi wengine wa kitanzania kutimiza ndoto zao za kufikia elimu ya juu.

"Tuendelee kushirikiana katika kuwasisitiza waajiriwa waliopo katika maeneo yetu ambao ni wanufaika ili waweze kurejesha mikopo yao kwa wakati …sote tuwe mabalozi kwa kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kurejesha mikopo", alisema Dkt. Kiwia.

Naye Mkurugenzi wa Urejeshaji na Urejeshawaji Mikopo, CPA(T) George Mziray aliwaeleza waajiri kuwa HESLB imeendelea kuboresha mifumo yake ya urejeshaji mikopo ili kuwawezesha waajiri na wanufaika kukamilisha taratibu zote kupitia kwenye mifumo bila kulazimika kufika ofisi za HESLB.

"Tuna mifumo ya wanufaika mmoja-mmoja (LIPA), ya waajiri wanaofuata sheria (EPO) na pia kwa ajili ya waajiri ambao hawafuati sheria (COPO) ili kuwawezesha kulipa kiasi walichoelekezwa", alisema Mziray.

> *Tuna mifumo ya wanufaika mmoja-mmoja (LIPA), ya waajiri wanaofuata sheria (EPO) na pia kwa ajili ya waajiri ambao hawafuati sheria (COPO) ili kuwawezesha kulipa kiasi walichoelekezwa, alisema Mziray.*

Katika hafla hiyo iliyofanyika katika Ukumbi wa Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA) uliopo katika Jengo la Michenzani Mall, Zanzibar, Taasisi zilizotunukiwa ni Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Wizara ya Afya, Ofisi ya Rais: Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Shirika la Viwango Zanzibar (ZBS), Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) na Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar. Taasisi nyingine ni ASA Microfinance Zanzibar Limited, DNATA Zanzibar Aviation Service Company Limited, Glorius Academy na Zanlink.

Awali, Meneja wa HESLB, Ofisi ya Zanzibar, Philbert Temba alisema kuwa taasisi nyingi za Zanzibar zinafanya vizuri katika marejesho lakini taasisi kumi zilizotunukiwa zimejipambanua zaidi kwa kuwasilisha majina ya wanufaika walioajiriwa, kukata 15% ya mishahara yao na kuwasilisha HESLB ndani ya siku 15 kama sheria ya HESLB inavyoelekeza.

Temba alisema kuwa taasisi hizo zimeenda mbele zaidi ya kutekeleza sheria, "siyo kwa kutimiza tu matakwa ya kisheria, lakini pia taasisi hizi zimekuwa na ushirikiano na mawasiliano ya karibu na HESLB kuhusu waajiriwa walionufaika na mikopo na kuhakikisha makato hayo yanafanyika mapema".

Hii ni mara ya pili kwa waajiri wa Zanzibar kutunukiwa ngao na HESLB kwa kutambua ushirikiano wao katika kurejesha mikopo ya elimu ya juu. Mara ya kwanza ilikuwa mwezi Aprili mwaka 2018 ambapo tuzo zilitolewa kwa taasisi tano zilizokuwa zimefanya vizuri kwa mwaka 2017/2018. Taasisi hizo zilikuwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Wizara ya Fedha na Mipango, Shule za Feza Zanzibar, Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA).



# JUMA:
## Asante Serikali kwa Samia Scholarship'

**Na Mwandishi Wetu**
**Dar es Salaam**

Juma Rubea Waziri, mwanafunzi wa mwaka wa pili wa Shahada ya Uhandisi wa Kompyuta na Teknolojia ya Habari (Computer Engineering and Information Technology) katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ameishukuru serikali kwa kubuni na kuanzisha fursa za 'Samia Scholarship'.

Juma ni mtoto wa mwisho kuzaliwa kati ya watoto sita wa familia ya Mzee Rubea Waziri yenye makazi yake jijini Tanga, na ni mtoto pekee katika familia hiyo aliyefanikiwa kufikia hatua ya elimu ya chuo kikuu.

Akielezea hali ya familia yake alipofanya mahojiano na jarida hili, Juma amesema kuwa baba yake anajishughulisha na uvuvi na mama yake anafanya shughuli za nyumbani na kusimamia malezi ya Watoto.

"Japokuwa baba kwa sasa ameanza kuzeeka, lakini ndio anayefanya shughuli kubwa ya kuhakikisha familia inapata mahitaji ya kila siku, kupitia kazi yake ya uvuvi, wakati mama akifanya shughuli za nyumbani na kutulea…"anaelezea Juma.

Juma alisoma katika Shule za Serikali kuanzia darasa la kwanza hadi alipohitimu kidato cha sita. Kwa upande wa kidato cha kwanza hadi cha nne alisoma katika Shule ya Sekondari Mwera iliyopo katika wilaya ya Pangani mkoani Tanga na kidato cha tano na sita alisoma katika shule ya Sekondari Minaki iliyopo Mkoa wa Pwani na kuhitimu kidato cha sita mwaka 2022 katika tahasusi ya Fizikia, Kemia na Hisabati (PCM).

Juma anasema pamoja na juhudi zake katika masomo ambazo zilimwezesha kupata ufaulu wa daraja la kwanza katika mitihani ya kidato cha sita (alama 4) na kupata ufadhili wa 'Samia Scholarship', anaishukuru Serikali kwa kuanzisha fursa hizo kwa kuwa zinachochea na kuhamasisha wanafunzi wanaosoma tahasusi za Sayansi kuongeza bidii ili kunufaika na ufadhili huo.

"Namshukuru Mungu, na naishukuru Serikali ya awamu ya sita kwa fursa za 'Samia Scholarship', na ninaahidi kusoma kwa bidii ili niendelee kunufaika na ufadhili huu hadi mwisho wa shahada yangu hii ya miaka minne…ninawasihi wanafunzi wa Sekondari wanaosoma masomo ya Sayansi, wasome kwa bidii ili nao wanufaike na ufadhili huu…"anasisitiza Juma.

Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (WyEST) ilianza kutoa ufadhili wa 'Samia Scholarship' ili kuongeza wataalamu na hamasa katika masomo hayo ya Sayansi. Kwa mara ya kwanza ufadhili huo ulitangazwa na Waziri wa Elimu, Sayansi ya Teknolojia Prof. Adolf Mkenda kwa mwaka wa masomo 2022/2023 na kunufaisha wanafunzi 640 waliokuwa na ufaulu wa juu zaidi katika tahasusi za sayansi (PCB, PCM, CBG, PGM, CBA, PMC na CBN) kwa kuzingatia mitihani ya kidato cha sita inayosimamiwa na Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA). Ili kunufaika na 'Samia Scholarship', wanafunzi husika ambao majina yao hutangazwa na WyEST, wanatakiwa kudahiliwa na kuendelea kusoma Shahada katika fani za Sayansi, Teknolojia, Uhandisi, Hisabati au Afya.



**Mei 03, 2024, Pretoria:** *Balozi James G. Bwana (aliyekaa kulia) katika picha ya pamoja na Menejimenti ya HESLB ikiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji Dkt. Bill Kiwia (aliyekaa kushoto) ambao walimtembelea Balozi ofisini kwake Pretoria nchini Afrika Kusini na kujadiliana kuhusu masuala ya kuongeza wigo wa utoaji na urejeshaji mikopo kutoka kwa watanzania walionufaika wanaoishi nje ya Tanzania.*



**Mei 09, 2024, Dodoma:** *Rais wa Jumuiya ya Wanafunzi wa Vyuo Vikuu na Vyuo vya Kati Tanzania (TAHLISO) Zainab Kitima (kulia) akipeana mkono na Maria John, rais aliyemaliza muda wake katika hafla ya uapisho wa kuingizwa madarakani rasmi baada ya kushinda katika uchaguzi uliofanyika Zanzibar Aprili 6, mwaka huu.*



**Mei 21, 2024, Dar es salaam:** *Menejimenti ya HESLB ikiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji, Dkt. Bill Kiwia (mwenye tai nyekundu) katika picha ya pamoja na ujumbe kutoka ECOBANK ukiongozwa na Charles Asiedua ambao walikutana na kujadiliana kuhusu namna ya kuboresha mashirikiano baina ya HESLB na Benki hiyo.*



**Mei 22, 2024, Dar es salaam:** *Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB Dkt. Bill Kiwia (kulia) akisalimiana na Kaimu Mkuu wa Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo (LST), Prof Sist Mramba mara baada ya kumaliza kikao kazi cha kujenga mashirikiano baina ya taasisi hizo mbili.*



**Mei 27, 2024, Tanga:** *Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda (katikati), Katibu Mkuu Prof. Carolyne Nombo (mwenye kofia nyeupe) pamoja na viongozi wengine wakifurahia uzinduzi wa Mwongozo wa Uombaji mkopo kwa mwaka 2024/2025, wa pili kulia ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya HESLB, Prof. Hamisi Dihenga na wa pili kushoto ni Mkurugenzi wa HESLB Dkt. Bill Kiwia.*




**Mei 29, 2024, Tanga:** *Maafisa wa HESLB wakiwahudumia wanafunzi waliofika kupata huduma katika banda la HESLB katika maadhimisho ya kitaifa ya Wiki ya Elimu, Ujuzi na Ubunifu yaliyofanyika katika viwanja vya shule ya Sekondari Popatlal.*



**Juni 12, 2024, Arusha:** *Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akimkabidhi cheti cha udhamini wa maonesho Meneja wa HESLB Kanda ya Arusha, Lucy Kirigha katika Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Taasisi ya Maboresho ya Serikali za Mitaa Tanzania (TOA) uliofanyika Juni 12 hadi Juni 14 mwaka huu.*

# Dirisha Maombi ya mikopo 2024/2025 lafunguliwa




Na Mwandishi
Dar es salaam.

HESLB imetangaza kufunguliwa kwa dirisha la maombi ya mikopo kwa wanafunzi kwa mwaka wa masomo 2024/2025 huku waombaji wakitakiwa kusoma mwongozo kabla ya kuomba.

Akizungumza na waandishi wa habari Juni 6, 2024 katika ofisi za HESLB jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Dkt. Bill Kiwia alisema Mei 27, 2024, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Adolf Mkenda alizindua miongozo mitano ya utoaji mikopo na ruzuku kwa mwaka wa masomo 2024/2025 inayopatikana kwenye tovuti ya Bodi ya Mikopo www.heslb.go tz na kuwasihi wanafunzi kusoma na kuelewa mwongozo husika kabla ya kujaza maombi mtandaoni.

"Niwakumbushe wanafunzi waombaji wa mikopo kwamba, HESLB imefungua rasmi dirisha la kuomba mkopo kwa njia ya mtandao kwa mwaka wa masomo 2024/2025 na lipo wazi kwa siku 90 kuanzia Juni 1 hadi Agosti 31, 2024." alifafanua Dkt. Kiwia.

Dkt. Kiwia alibainisha kuwa muda wa siku tisini unatosha kwa waombaji wa mkopo na kwamba maombi hayo yatafanyika kwa njia ya mtandao yaani https://olas.heslb.go.tz na kuwasisitiza wanafunzi waombaji mkopo kuandaa nyaraka muhimu zilizoainishwa kwenye miongozo.

"Tunasisitiza waombaji kuzingatia muda uliotolewa kwa kuwa hatutarajii kuongeza muda wa ziada baada ya Agosti 31, 2024. Pamoja na hilo wahakikishe majina ambayo mwombaji atakayojisajilia katika mfumo yanasomeka kwa mfanano na majina yaliyopo katika namba yake ya mtihani wa Taifa wa kidato cha nne," amesema Dkt. Kiwia.

Aidha, Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB alisisitiza kwamba kila mwombaji mkopo atapaswa kuwa na akaunti ya benki ili kurahisisha malipo akiwa chuoni na pia kwamba kwa waombaji wenye namba za NIDA watapaswa kuzijaza wakati wa kuomba mkopo.

Pamoja na mambo mengine waombaji wa mkopo wamesisitizwa kusoma na kuzingatia maelekezo yaliyomo katika miongozo ya utoaji mikopo na ruzuku ambayo tayari imewekwa katika tovuti ya HESLB ikiwa katika ya lugha ya Kiswahili na Kiingereza.

Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali imetenga TZS 787 Bilioni kwa ajili ya mikopo na ruzuku kwa jumla ya wanafunzi 250,000 ambapo idadi hiyo imeongezeka kutoka wanafunzi 224,056 mwaka 2023/2024 kwa jumla ya wanafunzi 25,944.

*"Niwakumbushe wanafunzi waombaji wa mikopo kwamba, HESLB imefungua rasmi dirisha la kuomba mkopo kwa njia ya mtandao kwa mwaka wa masomo 2024/2025 na lipo wazi kwa siku 90 kuanzia Juni 1 hadi Agosti 31, 2024." alifafanua Dkt. Kiwia.*

# WASILIANA NASI;

## DODOMA

Jengo la PSSSF,
Br. Makole, eneo la
Uhindini
S.L.P 984, Dodoma
Simu +255 758 067577
+255 739 06757
Barua Pepe:
info@heslb.go.tz

## ARUSHA

NSSF Jengo la Mafao,
Ghorofa ya Kwanza
S.L.P 2712,Arusha
Simu: 027 2520128
0624 100 011
0739 102 016
Barua Pepe:
arusha@heslb.go.tz

## MWANZA

PSSSF Plaza, ghorofa
ya pili Br. Kenyatta
S.L.P 3051, Mwanza
Simu: 028 2506008
0759 819 350
0738 153 661
Barua Pepe:
mwanza@heslb.go.tz

## ZANZIBAR

Jengo la Michenzani Mall,
Eneo la Michenzani
Ghorofa ya Tano
S.L.P 900,Zanzibar,
Simu: 0779 321 424
Barua Pepe:
zanzibar@heslb.go.tz

## HUDUMA KWA WATEJA

PSSSF Twin Tower
Ghorofa ya chini Mtaa wa Misheni
S.L.P 76068, Dar es Salaam
Simu: +255 758 067 577
+255 739 067 577
Barua Pepe:
info@heslb.go.tz

## MBEYA

Jengo la CAG, Ghorofa ya
Nne, Br. Mbalizi
S.L.P 319, Mbeya
Simu: 0738 131 310
0738 131 311
Barua Pepe:
mbeya@heslb.go.tz

## MTWARA

NHC Raha Leo Complex,
Ghorofa ya pili,
Kitalu Na. 217, Block H, Karibu
na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa
S.L.P: 969, Mtwara.
Simu: +255 733 068 171
Barua Pepe:
mtwara@heslb.go.tz

## DAR ES SALAAM

Bodi ya Mikopo ya
Wanafunzi wa Elimu ya Juu,
1 Mtaa wa Kilimo,Tazara,
Br. Mandela
S.L.P 76068,15471
Dar Es Salaam
Simu: 0736 665 533
Barua Pepe:
info@heslb.go.tz

#WeweNdoFuture
#TimizaWajibu
www.heslb.go.tz